

# **Haki ya mtoto asiyesikia kukua akifahamu lugha mbili**

The Swahili translation of

“The right of the deaf child to grow up bilingual”

by François Grosjean

University of Neuchâtel, Switzerland

Translated by Eunice Gladice Amolo

This translation was made possible by a collaborative project between the University of Neuchâtel, Switzerland (Language and Speech Laboratory) and Gallaudet University (Signs of Literacy Program) and was funded by The Parthenon Trust and the Elysium Foundation.

# Haki ya mtoto asiyesikia kukua akifahamu lugha mbili

Francois Grosjean  
University of Neuchatel, Switzerland

Kila mtoto asiyesikia, hata kiwango chake cha kutosikia kiwe cha aina gani, anapasa kuwa na haki ya kukua akifahamu lugha mbili. Kwa kufahamu na kutumia lugha ya alama na ile ya maongezi (katika maandishi na ikiwezekana katika mfumo wake wa matamshi), mtoto atakuwa na uwezo kamili wa utambuzi, na kuelewa zaidi ya lugha moja ili aweze kutangamana vilivyo na jamii.

## Ni mambo gani mtoto anahitaji kutimiza kwa matumizi ya lugha?

Mtoto asiyesikia anahitajika kutimiza mambo kadhaa kwa kutumia lugha:

1. Kuwasiliana na wazazi na jamaa haraka iwezekanavyo. Mtoto anayesikia kwa kawaida hufahamu lugha akiwa angali mdogo ili mradi tu awe atasikia watu wakiongea na aweze kuelewa. Lugha kwa hivyo ni njia moja wapo muhimu ya kuimarisha uhusiano na kuunganisha jamii na kuleta uhusiano wa karibu kati ya mtoto na wazazi wake. Kile kilicho cha kweli kwa mtoto anayesikia ni sharti kiwe cha kweli kwa mtoto kiziwi. Mtoto ni sharti aweze kuwasiliana na wazazi wake kwa njia ya lugha ya kiasili haraka na kwa ukamilifu iwezekanavyo. Ni kupitia lugha ambapo uhusiano kati ya mzazi na mtoto unaimarika.

2. Kupata uwezo wa ufahamu wakiwa wangali wachanga. Kupitia lugha mtoto hupata maarifa ya ufahamu ambayo ni muhimu katika kuimarika kibinafsi. Miongoni mwa haya tunapata aina mbali mbali za kufikiria, kufupisha na kukumbuka n.k. Kutokuwepo kabisa lugha, kujifunza lugha isiyo ya kiasili au matumizi ya lugha ambayo haitambuliki au kufahamika kunaweza kuwa madhara mabaya kwa ustawi wa ufahamu kwa mtoto.

3. Kupata elimu ya ulimwengu. Mtoto ataweza kufahamu mengi ulimwenguni hasa kupitia lugha. Wakati anapowasiliana na wazazi wake, watu wengine katika jamaa, watoto na watu wazima, habari kuhusu ulimwengu zitazungumziwa na ataweza kufahamu mengi ya ulimwengu. Ni kupitia elimu hii ambapo mtoto huwa na msingi wa mambo atakayojifunza shuleni. Pia ni elimu hii ya ulimwengu inayomfanya mtoto kufahamu lugha kwa undani zaidi; mtoto hawezi kufahamu lugha kikamilifu bila msaada wa elimu hii.

4. Kuwasiliana kikamilifu na wale waliokaribu. Mtoto asiyesikia anapaswa kuwa na uwezo wa kuwasiliana kikamilifu na wale anaohusiana nao (wazazi, ndugu zake, marafiki, walimu, watu wazima n.k.). Mawasiliano yanapasa kufanyika kupitia kiwango cha juu cha habari katika lugha inayostahili kwa mwenye kushiriki kwenye mazungumzo na hali ilivyo wakati wa mazungumzo hayo. Wakati Fulani itakuwa lugha ya ishara, wakati mwingine iwe lugha ya kuongeza (katika moja ya mitindo yake), na wakati mwingine lugha zote mbili zitumike.

5. Kuzoea lugha zote mbili. Kupitia lugha, mtoto asiyesikia ni sharti aweze kutangamana na wale wasiosikia na wale wanaosikia. Anapasa kutambua kwa kiwango fulani na awe na uwezo wa kuwasiliana na wale wanaosikia hasa wazazi wake, watu wengine katika jamaa yake (90% ya watoto wasiosikia wana wazazi wanaosikia). Lakini hata hivyo mtoto huyo anapaswa kujifahamisha mapema maishani lugha ya viziwi. Mtoto huyo ni sharti aridhike na maisha aina zote mbili na kadhalika aweze kufahamu aina hizo mbiliipasavyo.

Kufahamu lugha mbili ndiyo njia ya pekee ya Kutimiza mahitaji haya.

Kufahamu zaidi ya lugha moja na matumizi ya mara kwa mara ya lugha hizo ndiyo njia ya pekee ambayo mtoto anayesikia anaweza kutimiza mahitaji yake, yakiwa ni; kuwasiliana mapema na wazazi wake, kuwa

na uwezo wa kufahamu, kujifunza mambo ya ulimwengu, kuwasiliana kikamilifu na wale aliokaribu nao na kuzoeana na wale wanaosikia na wasiosikia.

### **Ni aina gani ya ufahamu wa lugha mbili inayohitajika?**

Kufahamu lugha mbili kwa mtoto asiyesikia kunahusisha lugha ya alama inayotumiwa na jamii ya wasiosikia na lugha ya maongezi inayotumiwa na wengi wanaosikia. Lugha ya wanaosikia inaweza kufahamika katika mfumo wa maandishi na ikiwezekana katika mfumo wa matamshi. Lugha hizi mbili hutekeleza majukumu muhimu kulingana na mtoto mwenyewe: Watoto wengine hushindwa kutumia lugha ya alama, wengine nao hushindwa kutumia lugha ya maongezi ilihali wengine hutumia aina zote mbili. Kwa kuongezea, aina nyingi za ufahamu wa zaidi ya lugha moja zipo kutokana na kuwepo kwa viwango tofauti vya kutosikia na hali ya mawasiliano kupitia lugha hii iliyo na sehemu kadhaa (mbinu nne tofauti za lugha, mifumo miwili ya kuongea na miwili ya utambuzi n.k.). Haya yote yakiambatanishwa, mtoto asiyesikia atapata uwezo wa kutumia zaidi ya lugha moja na kuwa na utamaduni zaidi ya mmoja katika viwango tofauti. Kwa ajili ya haya, mtoto hatakuwa tofauti na takriban nusu ya idadi ya watu wote duniani wanaoishi wakifahamu zaidi ya lugha moja. (Imekadiriwa kwamba kuna watu wengi humu duniani leo wanaofahamu lugha mbili au zaidi kupita wale wanaofahamu lugha moja). Sawa na watoto wengine wanaofahamu zaidi ya lugha moja, mtoto asiyesikia ataweza kutumia lugha zake maishani na ataweza kutangamana kwa hali yoyote na wenzake wasiosikia na wale wanaosikia.

### **Lugha ya alama ina umuhimu gani?**

Lugha ya alama inapasa kuwa lugha ya kwanza (au moja ya lugha mbili za kwanza) ambayo mtoto ambaye kiwango chake cha kutosikia ni cha juu huielewa mapema. Hii ndiyo lugha ya kiasili inayofahamika kwa haraka na ambayo inahakikisha mawasiliano kamili. Kinyume na lugha ya maongezi, lugha ya alama humpa mtoto asiyekia nafasi ya kuwasiliana na wazazi wake kikamilifu na haraka, ikiwa ataifahamu mapema. Lugha ya alama hutekeleza jukumu muhimu katika ufahamu na kuimarika kwa mtoto asiyesikia na humsaidia kujifunza mambo mengi ya ulimwengu. Pia itamwezesha kuzoeana na wale wasiosikia (ambapo yeye ni mmoja wa tabaka hilo) mara tu anapotangamana nao. Kwa kuongezea, lugha ya alama itamwezesha mtoto huyo kuielewa lugha ya maongezi, iwe katika mfumo wake wa maandishi au wa matamshi. Inafahamika wazi kwamba lugha ya kwanza inapoeleweka vyema, iwe ya alama au ya maongezi, humwezesha mtu kuielewa lugha ya pili kwa urahisi. Mwisho kabisa, mtoto akiweza kutumia lugha ya alama ni thibitisho kwamba mtoto huyo ameelewa angalau lugha moja. Licha ya juhudi za mtoto asiyesikia na wale wataalam walio karibu naye na matumizi ya vifaa mbali mbali vya kitaalam, ni dhahiri kwamba watoto wengi wasiosikia huwa na matatizo katika kuongea na kuielewa lugha ya maongezi katika mfumo wake wa matamshi. Kumuacha mtoto akae muda mrefu akisubiri aweze kuongea ni sawa na kumnyima mtoto asiyesikia nafasi ya kujifunza lugha mapema na kwamba mtoto huyo atachelewa kuimarika kiufahamu, kilugha na kibinafsi.

### **Lugha ya maongezi ina jukumu gani?**

Kufahamu zaidi ya lugha moja kunamaanisha kujua kutumia lugha mbili au zaidi. Lugha nyingine kwa mtoto asiyesikia ni ile ya maongezi inayotumiwa na wale wanaosikia ambapo yeye pia ni mmoja katika jamii hiyo. Lugha hii katika mfumo wake wa matamshi au maandishi ndiyo lugha ya wazazi wake, kaka zake, dada zake, jamaa zake marafiki wake wa baadaye, waajiri wake n.k. Iwapo wale wanaotangamana na mtoto huyo katika maisha ya kila siku hawaelewi lugha ya alama, hata hivyo ni jambo la muhimu kwamba mawasiliano yafanyike na hii inawezekana tu kupitia lugha ya maongezi. Ni lugha hii kupitia mfumo wake wa maandishi inayoweza kuwa njia ya kujipatia elimu. Mengi tunayojifunza huwasilishwa kwetu kupitia maandishi iwe nyumbani au kwa kawaida mara nyingi shuleni. Kwa kuongezea ni kwamba ufanisi wa kielimu na utaalum katika siku za usoni kwa mtoto asiyesikia utategemea zaidi kiufahamu kwake vyema lugha ya maongezi katika mfumo wake wa maandishi na ikiwezekana katika mfumo wa matamshi.

## Hitimisho

Ni jukumu letu sote kumpa nafasi mtoto asiyesikia kufahamu lugha mbili. Lugha ya alama kwa jamii ya wasiosikia (kama lugha ya kwanza ikiwa kiwango chake cha kutosikia ni cha juu) na ile inayotumiwa na wengi wanaosikia kama lugha ya pili. Ili aweze kuzifahamu lugha hizi mbili, mtoto anapasa kutangamana na jamii zote mbili na ni sharti ahisi haja ya kujifunza na kutumia lugha hizo. Kwa upande wa lugha ya maongezi, uimarikaji wa teknolojia unaifanya hali ya siku za usoni ya mtoto asiyesikia isiweze kubashirika. Teknolojia hiyo humfanya mtoto asiyesikia asiweze kuimarika kiufahamu, kibinafsi na kumweka katika hatari ya kutokuwa na haja ya kuzoeana na jamii hizo mbili ambapo yeye pia ni mmoja wao. Kujifahamisha mapema na lugha hizo mbili humpa mtoto hakikisho kuliko kufahamu tu lugha moja bila kujali hali yake ya baadaye itakavyokuwa na jamii atakayochagua kuishi. Mtu hawezi kujuta kwa kufahamu zaidi ya lugha moja lakini mtu anaweza kujuta akiwa hatafahamu mengi ya kutosha hasa ikiwa kuimarika kwake kuko hatarini. Mtoto asiyesikia anapasa kuwa na haki ya kukua akifahamu zaidi ya lugha moja na ni wajibu wetu kumsaidia kuzifahamu lugha hizo.

### Makala mengine yaliyoandikwa na mwandishi huyu

Grosjean, F. (1982). *Kuishi ukifahamu lugha mbili: Utangulizi wa Lugha Mbili* Cambridge, Ma: Harvard University Press.

Grosjean, F. (1987). Bilingualism. In *Ensaiklopedia ya Galaudet kuhusu Watu wasiosikia na Kutosikia*. New York: McGraw.Hill.

Grosjean, F. (1992) Mtu anayefahamu lugha mbili na tamaduni mbili katika ulimwengu wa wanaosikia na wasiosikia. *Mafunzo kuhusu Lugha ya Alama*, 77, 307-320.

Grosjean, F. 1994). Ufahamu wa Lugha Mbili. Katika *Ensaiklopedia ya Lugha na Lugha Nyingi*. Oxford: Pergamon Press.

Grosjean, F. (1994). Alama za lugha mbili: Maswala katika *Ensaiklopedia ya Lugha na Lugha Nyingi*. Oxford: Pergamon Press.

Grosjean, F. (1996). Kuishi kwa kufahamu Lugha mbili na Tamaduni mbili. Katika Mafunzo ya I. Parasnis (Ed.), *Uzoefu wa Lugha na Tamaduni tofauti tofauti: Akisi kuhusu Uzoefu wa Kutosikia* (pp. 20-37) Cambridge: Cambridge University Press.